# Udhibiti wa kulazimisha
## Jua dalili za unyanyasaji (Coercive control)

**Udhibiti wa kulazimishwa ni wakati mtu anaumiza, anatisha au anamtenga mtu mwingine mara kwa mara ili kumdhibiti. Ni unyanyasaji wa nyumbani na inaweza kusababisha madhara makubwa.**

## Kuhusu udhibiti wa kulazimisha

### Ni muundo unaoendelea na unaorudiwa wa tabia

Baadhi ya tabia za kulazimisha na kudhibiti zinaweza kuonekana kuwa ndogo zenyewe, lakini zinaporudiwa au kuendelea, zinaweza kusababisha madhara makubwa.

### Inajumuisha tabia za kimwili na zisizo za kimwili

Inaweza kujumuisha tabia yoyote ambayo inatisha, inaumiza, inatenga au inadhibiti mtu mwingine. Inaweza kujumuisha unyanyasaji wa kimwili na unyanyasaji wa kijinsia, lakini si lazima.

### Uzoefu wa kila mtu ni tofauti

Mtu mnyanyasaji mara nyingi hurekebisha tabia ya kudhibiti kulingana na mtu anayemdhulumu. Inaweza kubadilika kwa wakati.

### Inaweza kutokea katika aina tofauti za mahusiano

Inaweza kutokea wakati watu wanaochumbiana isivyo  kirasmi, katika uhusiano wakimahaba mzito au wanaotengana. Mtu anayetukana pia anaweza kuwa mwanafamilia, mkazi mwenza au mlezi.

Udhibiti wa kulazimishwa ni mbaya katika uhusiano wowote, lakini kuanzia tarehe 1 Julai 2024, ni kosa la jinai katika NSW wakati mtu anatumia tabia hizi kuelekea mshirika wa karibu wa sasa au wa zamani kwa nia ya kuwalazimisha au kuwadhibiti.

### Ni makusudi

Kila wakati mtu anatumia mienendo ya unyanyasaji, anafanya uamuzi wa kufanya hivyo, na anawajibika kwa unyanyasaji wao na matokeo yake.



NSW GOVERNMENT

# Mifano ya tabia za unyanyasaji

Hii ni baadhi tu ya mifano ya tabia za kulazimisha na kudhibiti:

- Kudhuru afya ya akili ya mtu kimakusudi au ustawi wa kihisia, kwa mfano, kutukana na kumkosoa mtu kila mara.
- Kuaibisha, kufedhehesha au kudharau mtu kwa mfano, kushiriki habari za faragha kumhusu au kufanya vicheshi ambavyo vinadhuru kujistahi na utu wao.
- Kutumia vurugu ili kuumiza, kudhibiti au kutisha mtu kwa mfano, kuumiza mtu kimwili kwa njia yoyote ile, kurusha au kuvunja vitu, au kuendesha gari bila kujali ili kumfanya mtu ajisikie hana usalama.
- Kutoa vitisho kwa mfano, kutishia kuondoa udhamini wa visa.
- Kumtenga mtu kutoka kwa marafiki, familia na jumuiya kwa mfano, kuchukua simu ili asiweze kuwasiliana na familia na marafiki.
- Kuweka kikomo uhuru na kujitegemea kwa mtu au kudhibiti chaguzi zao za kila siku kwa mfano, kuweka sheria kuhusu kile anachoweza kuvaa au kumzuia mtu huyo kutoka nje ya nyumba au kutoka peke yake.
- Kudhibiti au kupunguza ufikiaji wa mtu kwa pesa au uwezo wake wa kupata pesa kwa mfano, kutomruhusu kufanya kazi nje ya nyumba ili kupata pesa.
- Kuchunguza kwa makini au kufuatilia matendo mtu, mawasiliano au mienendo ya mtu ana kwa ana au mtandaoni kwa mfano, kusoma barua pepe zao na jumbe za maandishi bila idhini yao.
- Kumtenga mtu kutoka kwa tamaduni au jamii yake au kumzuia asieleze utambulisho wake wa kitamaduni au kiroho kwa mfano, kutomruhusu kuzungumza lugha yao ya kitamaduni.
- Kushinikiza au kulazimisha mtu kufanya ngono au kudhibiti uchaguzi wao wa uzazi kwa mfano, kuweka sheria kuhusu wakati lazima mtu afanye ngono.
- Kutumia mifumo, huduma na michakato ya kutishia, kudanganya au kudhibiti mtu mwingine kwa mfano kutoa ripoti za uwongo kwa huduma za ulinzi wa watoto au uhamiaji.

# Udhibiti wa nguvu na sheria

Kuanzia tarehe 1 Julai 2024, **udhibiti wa shuruti ni kosa la jinai katika NSW** mtu anapotumia tabia hizi kwa mshirika wa karibu wa sasa au wa zamani kwa nia ya kuwashurutisha au kuwadhibiti. Sheria itatumika tu kwa tabia ya unyanyasaji itakayotokea baada ya tarehe 1 Julai 2024.

Jua zaidi kuhusu hatua za Serikali ya NSW juu ya kuharamisha udhibiti wa shuruti.

Iwe unapitia udhibiti wa kulazimishwa kutoka kwa mshirika wa karibu, mwanafamilia, mlezi, au mtu mwingine yeyote, daima si sawa na kuna usaidizi unaopatikana.

# Pata msaada

**Ikiwa uko katika hatari ya mara moja**, piga Sifuri Tatu **[000]** na uombe Polisi.

**Ikiwa unahitaji mkalimani**, pigia Translating and Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani) kwa nambari **131 450** na uwaombe kuwasiliana na huduma ambayo ungependa kuzungumza nayo.

**Ikiwa wewe au mtu unayemjua anapitia udhibiti wa kulazimishwa**, piga 1800RESPECT **( 1800 737 732 )** au tembelea 1800respect.org.au/languages kwa msaada na taarifa. Inapatikana kwa saa 24, siku 7 kwa wiki.

**Ikiwa una wasiwasi kuhusu tabia yako**, piga Men's Referral Service (Huduma ya Rufaa ya Wanaume) kwenye **1300 766 491**. Inapatikana kwa saa 24, siku 7 kwa wiki. Hii ni huduma ya bure, ya siri na isiyojulisha jina la mtu.

**Ikiwa unahitaji ushauri wa kisheria au usaidizi**, piga LawAccess NSW kwa **1300 888 529** kati ya 9am hadi 5pm, Jumatatu hadi Ijumaa.

Taarifa zaidi kuhusu udhibiti wa kulazimisha na huduma za usaidizi zinapatikana kwa Kiingereza kwenye **nsw.gov.au/coercive-control**



NSW GOVERNMENT